OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHURI YA MJI NJOMBE.

SHULE YA SEKONDARI MATOLA,
S.L.P 169,
NJOMBE.
.....

BARUA PEPE: gideon.massao@yahoo.com.
NAMBA YA SIMU: 0755684800/0755187814.
Kumb. Na MTSS/J.1/VOL.II/30.

JINA LA MWANAFUNZI.....
.....
S.L.P .....
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MATOLA KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

1.0 UTANGULIZI.

Nina furahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na **kidato cha kwanza** katika shule ya sekondari ya **MATOLA mwaka wa masomo 2021.** Shule ipo umbali wa kilometa 65 kusini mwa Halmashauri ya mji njombe. Usafiri wa basi kutoka mjini NJOMBE unapatikana katika kituo cha mabasi cha NJOMBE, nauli ni TSHS 5,000/=. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2020. Hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 10/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 23/01/2021 ndani ya siku kumi na nne (baada ya hapo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine).

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 SARE ZA SHULE.

(a) Sare ya shule hii ni:

1. **WAVULANA.**
   a. **DARASANI**.
   - Mashati mawili meupe (Tetroni) mikono mirefu.
   - Suruali mbili moja rangi ya daki bluu na nyingine damu ya mzee.
   - Soksi rangi nyeusi jozi mbili.
   - Sweta mbili (moja damu ya mzee na nyingine rangi ya kijivu (grey) ziwe za **KUFUMWA SIO MKENYA AU INDIA.**
   - Mkanda mweusi(WANGOZI), viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi jozi mbili kwa ajili ya darasani.
   - Suruali nyeusi kwa ajili ya kazi za nje.
   - Pull neck rangi ya kijivu.
   - NGUO ZA NDANI ZAKUTOSHA (KUANZIA TANO NA KUENDELEA
   - Saa ya mkononi kwa matumizi yake ni lazima kwasababu shule hakuna matumizi ya kengele.

b. MICHEZO.

- Viatu vya michezo aina yoyote
- **Track suit rangi ya Light blue (bluu bahari)**
- Tisheti rangi ya bluu. (IWE NZITO)
- Bukta rangi ya bluu.

2. **WASICHANA**:

A. DARASANI

- Suruali mbili (moja rangi ya damu ya mzee na nyingine rangi ya Daki bluu (dark blue) ANGALIA KIAMBATISHO KWAAJILI YA MSHONO.
- Mashati mawili meupe mikono mirefu(Tetroni).
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (FREE SIZE)
- Sweta mbili (moja damu ya mzee na nyingine rangi ya kijivu (grey) ziwe za **KUFUMWA SIO MKENYA AU INDIA.**
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi jozi mbili kwa ajili ya darasani.
- Sketi nyeusi kwa ajili ya kazi za nje.
- Pull neck rangi ya kijivu.
- NGUO ZA NDANI ZAKUTOSHA (KUANZIA SABA NA KUENDELEA
- TAULO ZA KIKE (PEDI) za kutosha.
- Saa ya mkononi kwa matumizi yake ni LAZIMA KWASABABU SHULE HAKUNA MATUMIZI YA KENGELE.

B. MICHEZO.

- **Viatu au** Raba za michezo.
- Tisheti rangi ya Bluu.
- **Track suit rangi ya Light blue (bluu bahari)**
- Tisheti rangi ya bluu. (IWE NZITO)
- Bukta rangi ya bluu.

2.2 VIFAA VINGINE VYA DARASANI.

- Daftari (Kaunta) za kutosha masomo kumi atakayosoma.
- Mkebe wenye Vifaa vya Hisabati, kalamu ya risasi (Penseli), kalamu za wino za kutosha.
- Kamusi ya kingereza kwa kingereza moja (Dictionary – English to English) ni muhimu.
- Bunda (rimu) moja la karatasi A4 kwaajili ya matumizi yake **(LILILOANDIKWA (NO.1 MONDI)**
- Faili gumu kwaajili ya kuhifadhia karatasi zake za mazoezi na majiribio mbalimbali.

2.3 . MAHITAJI YA HOSTELI KWA WOTE.

a) Godoro moja la futi $2\frac{1}{2}$ (mbili na nusu) inchi 3, uje nalo.

b) Blanketi moja.

c) Shuka mbili (Wavulana rangi ya bluu bahari na wasichana rangi ya pink.

d) Ndoo moja ya plastiki ya lita kumi kwa matumizi yake binafsi.

e) Vyombo vya kulia chakula yaani, sahani, bakuli, kijiko na kikombe.

f) FEDHA YA HUDUMA YA KWANZA **TSHS 10,000/= kwa mwaka (ilipwe benki)**

g) Begi Madhubuti kwaajili ya kuhifadhi mahitaji yake.

h) Taulo moja kwa wavulana

i) Kanga au kitenge kwa wasichana

j) Mto

k) Jembe lenye mpini moja (wasichana)

l) Panga moja (wavulana)

NB: 1. Usikabidhi vitu vyako kwa Mwanafunzi, mpaka upate maelekezo kutoka kwa mwalimu.

2. Nguo za nyumbani hazirihusiwi hapa shuleni hivyo asije nazo kamwe.
3. Mwanafunzi asije na vyakula vilivyopikwa au vibichi kutoka nyumbani.
4. Haruhusiwi kuja na vipodozi vya aina yoyote.

2.4. UTARATIBU WA KUTOA CHAKULA SHULENI.

Wazazi waliafiki kuwa watoto wao wapate chakula milo yote mitatu. Hivyo michango ya chakula ni kama ifuatavyo:-

a) Mahindi debe 12 (kumi na mbili) yaani kilo 240 kwa mwaka, Debe 6 kwa nusu muhula yaani kilo 120 kila muhula.

b) Mchele kilo 20 yaani debe moja kwa mwaka, hivyo kwa nusu muhula ni nusu debe au kilo 10

c) Maharage kaki debe 2.5 (mbili na nusu)kwa maka

d) HOSTELI TSHS 136,000/=kwa mwaka, TSHS 68,000/= kwa nusu muhula

- **Ulete bidhaa yaani mahindi, maharage) yawe katika hali nzuri na mchele (supa) na usilete fedha.**
- **Michango ya fedha ilipwe benki ya NMB akaunti namba 60610003731 (MATOLA SEKONDARI), jina la akaunti Recurrent accoun**t**. LETA RISITI YA MALIPO(BPS**) **ikiwa na jina la mwanafunzi na Kidato anachosoma mwanafunzi**.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na OFISI YA RAIS - TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
e) Kufahamu mpaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA/ KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamizito/ kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) KUMILIKI KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU. HIVYO NI MARUFUKU KUJA NA SIMU SHULENI.

3.2.MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA WANAFUNZI.

a) Medical Examination fomu ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

TANBIHI:

(i) kubadili jina, ila kwa sababu maalumu kwa kuapa mahakamani.
(ii) Kubadili Dini bila idhini ya mzazi au mlezi wake.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
MKUU WA SHULE
GIDEON D MASSAO
0755 684 800

OFISI YA RAIS (OR) TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI MATOLA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI

1. **MWANAFUNZI.**

Jina la mwanafunzi.....
Anuani
……..
Nimekubali/Sijakubali kujiunga na jumuiya ya shule ya sekondari ya Matola. Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa. Ninaahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria na taratibu za shule kama tunavyoelekezwa.

Sahihi ya mwanafunzi ……..
Tarehe …….

2. **<u>MZAZI/MLEZI</u>**

Mimi
……
Mzazi/Mlezi wa ……
Nimesoma kwa makini maagizo yaliyotolewa yanayohusu mtoto wangu.
Nimekubali/Sijakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo.

Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu **kielimu** na **kimalezi.**

Sahihi ya mzazi/mlezi …….
Tarehe ……

OFISI YA RAIS (OR) TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI MATOLA.

MAELEZO BINAFSI:-

1. Jina lako ……. Kidato cha ……. Tarehe ya kuzaliwa ……. Mahali ulipozaliwa …… Wilaya Dhehebu …….. Shule ya msingi ulikotoka ……

2. **BABA**
   a) Jina la baba……..
   b) Yu hai/amefariki ……
   c) Anuani yake kama yu hai …….
   d) Kazi yake ……
   e) Ameajiriwa na idara gani?.....
   f) Dini ya baba ni ……
   g) Namba ya simu ……..

3. **MAMA**

a) Jina la mama……..
b) Yu hai/amefariki ……
c) Anuani yake kama yu hai …….
d) Kazi yake ……
e) Ameajiriwa na idara gani?.....
f) Dini ya mama ni ……
g) Namba ya simu ……..

4. **MLEZI**
   Unaye mlezi, Mlezi ni mtu yeyote ambaye si mzazi wako lakini anakutunza na kukulipia gharama zote za mahitaji yako) NDIO/HAPANA.
   Kama jibu ni ndio:-

a) Jina la Mlezi …….
b) Uhusiano na mlezi (Mjomba,Shangazi,kaka n.k)……
c) Anuani yake ……..
d) Dini ya mlezi ……
e) Kazi yake ……
f) Ameajiliwa na idara gani? ……
g) Namba ya simu ……..

5. **ANUANI YA BABA AU MAMA AU MLEZI ATAKAYEKUWA ANAWASILIANA NA SHULE.**
   …….
   ……
   NAMBA YA SUMU …….
   JINA NA SAHIHI YAKE …….

OFISI YA RAIS (OR) TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI MATOLA
SHERIA ZA SHULE.

1. Mashutumu,matusi na kupigana ni marufuku.
2. Mwanafunzi ni lazima awe mtii na mwenye heshima kwa mkuu wa shule, walimu, watumishi wasio walimu na watu wote kwa ujumla wakati na mahali popote ndani na nje ya shule.
3. Mwanafunzi atatakiwa kuhudhuria vipindi vyote darasani,nje ya darasa na kazi zote za mikono kwa muda wote wa masomo yake.
4. Mwanafunzi atasimama (ikiwa alikaa) na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote.
5. **Mwanafunzi anatakiwa kuongea lugha ya kiingereza wakati wote awapo shuleni**.
6. Nimarufuku mwanafunzi kuvuta sigara, bangi, kunywa pombe, madawa ya kulevya , kuleta vileo shuleni au kuonekana mahali penye ulevi wakati wote wa masomo.
7. Wizi wa aina yoyote ni kosa kubwa, adhabu ni kufukuzwa shule na kupelekwa mahakamani.
8. Nimarufuku mwanafunzi yeyote kujihusisha na uasherati awapo mahali popote kwa muda wake wa masomo.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea maeneo ya ofisi ya mkuu wa shule, ofisi ya walimu,nyumba za walimu na wafanyakazi ila kwa kibali maalumu.
10. Nimarufuku mwanafunzi kuoa au kuolewa, kupata au kusababisha mimba au kutoa mimba.
11. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule awapo darasani,kwenda hospitali, maandamano halali, kusafiri kuja na kurudi nyumbani na mahali popote atakapo ruhusiwa.
12. **Mwanafunzi haruhusiwi kupaka manukato, kupaka rangi za mdomo na kucha, kuvaa kofia, viatu vya ghorofa, kidani, mkanda mpana, kuvaa hereni, pete, mkufu awapo shuleni.**
13. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu, kuwa na kucha ndefu, nywele ndefu. Hairuhusiwi kunyoa nywere mtindo wa denge/punk. Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele mtindo wowote
14. Vifaa vyote vya shule ni mali ya umma mwanafunzi hana budi kuvitunza kwa uangalifu. Uharibufu wa makusudi wa aina yoyote ni marufuku na lazima kulipia uhalibifu unao tokea.
15. Upigaji kelele na soga mahali popote penye mkusanyiko rasmi darasani, msitari, “parade” nk. Ni marufuku.
16. Nimarufuku mwanafunzi kuendesha shughuri za vyama vya siasa shuleni. Vilevile mwanafuzi haruhusiwi **kuvaa mavazi yanayotumiwa na chama chochote cha siasa**.
17. Mwanafunzi anayefikiwa na mgeni ni budi amtaarifu mwalimu wa zamu.
18. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki/kuwa na simu muda wote awapo shuleni. Akikutwa nayo atanyang’anywa na kufukuzwa shule

MEDICAL CERTIFICATE FORM.

To be completed by the medical officer in respect of form on entrants.
Pupil's full name …….
Age ……..year ……
sex……..
Blood Count (Red and White)
…….
Stool Examination ……..
Urine Analysis
…….
Syphilis
……
T.B Test
……
EyeTest……
Ears
……
Chest
……
Spleen
……
Abdomen
……

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical defects or impairments chronic or family diseases.
……
……
……
……
……
……
……

I certify that the above is fit/unfit for admission into day/boarding school.
Signature …….
Designation …….
Station ……..
Date ……. Stamp …….